**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MKUU WA MKOA WA RUVUMA**




# JARIDA LA RS RUVUMA TOLEO LA PILI APRILI 2024

www.ruvuma.go.tz

rs ruvuma

# KARIBU MKOA WA RUVUMA



Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupigachapa, kutoa nakala kivuli au kutoa baadhi ya maandishi ya Jarida hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Mwandishi kwa maandishi.

Jarida limehaririwa na **Albano Midelo** wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

**YALIYOMO**

1.RC Ruvuma awafariji yatima 74 Chipole Songea
2.Kanali Abbas aipongeza Manispaa ya Songea
3.Wakurugenzi walivyokabidhiana ofisi Songea
4.Serikali yaiboresha hospitali ya Mpitimbi
5.RC Ruvuma ahimiza kasi ukusanyaji mapato
6.RAS Ruvuma awafunda watumishi wa umma
7.RC aiagiza Madaba kutekeleza maagizo ya LAAC
8.Muonekano wa jengo la Halmashauri ya Madaba
9.Bandari ya kimkakati ya Ndumbi ziwa Nyasa
10.Wakulima Mbinga kuzalisha kahawa tani 20,000
11.kisiwa cha Mbambabay chenye utajiri wa samaki wa mapambo
12.Peramiho ilivyosheheni utalii wa kihistoria
13.Usiyoyajua kuhusu kisiwa cha Lundo
14.Bwawa la viboko kivutio adimu Namtumbo
15.Daraja la Mitomoni kuanza kujengwa Juni 2024
16.Bilioni 34 zilivyoboresha sekta ya elimu Ruvuma
17.Serikali yatoa milioni 826 kukamilisha miundombonu ya elimu Tunduru
18.Hospitali ya Tunduru ilivyoboresha huduma za afya
19.Elimu ilivyopunguza madhara ya tembo Namtumbo
20.DC Nyasa awaasa wananchi kujitokeza uchaguzi serikali za mitaa
21.Ofisi ya RC Ruvuma yapokea mipira 1,000 toka TFF
22.Wadau Namtumbo wadhamiria kusimamia mfumo wa stakabadhi
23.Milioni 69 kujenga kituo cha askari wanyamapori Namtumbo
24.Serikali yafikisha umeme vijiji 81 Nyasa
25.NFRA yawafunda wakulima Songea
26.Dkt.Nchimbi akabidhi vifaa vya usafiri kwa viongozi Madaba
27.Katibu Mkuu CCM aagiza uwekezaji kwenye michezo
28.Madaktari bingwa kutoa huduma za kibingwa Songea
29.Mbinga wavunja rekodi mapokezi ya Katibu Mkuu CCM

30.Katibu Mkuu CCM alivyopokewa kimila na wazee wa Songea
31.Dkt.Nchimbi azuru kaburi la Muasisi wa TANU Mbinga
32.Katibu Mkuu CCM azuru kaburi la Kepteni Komba Lituhi
33.Wanawake 6.500 hufariki kila mwaka kwa saratani
34.Wezi ndani ya magari wanaswa Songea

# TAHARIRI

Wapendwa wasomaji wetu ninayoheshima kubwa kuwaalika katika Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kusoma habari na makala mbalimbali ambazo zinakuwa zinachapishwa na jarida hili.

Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikali kuhakikisha kila mwezi GCU Mkoa na Halmashauri zake zinachapisha jarida ili kutangaza shughuli mbalimbali zinazofanywa na serikali ikiwemo kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, mahusiano na kutangaza fursa za utalii na uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma na namna viongozi wanavyosikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Furahia kusoma

# MKUU WA MKOA WA RUVUMA  AWAFARIJI YATIMA 74 CHIPOLE




Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abass Ahmed ametoa msaada wa vitu mbalimbali vyenye thamani ya Zaidi ya shilingi laki nane na fedha taslimu shilingi 690,000 kwa kituo cha Watoto yatima Chipole wilayani Songea.

Kituo hicho chenye Watoto yatima 74 kinamilikiwa na watawa wa Shirika la Mtakatifu Agnes Jimbo Kuu katoliki la Songea.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo,Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Abbas amevitaja vitu walivyopewa Watoto hao kuwa ni  mchele kilo 100,maharage kilo 50,mafuta ya kupikia lita 20,sukari kilo 50,unga wa mahindi kilo 50 na sabuni ya unga mifuko miwili.

“Mimi binafsi  nimekuwa na utamaduni katika maisha yangu,nikipata fursa huwa natembelea vituo vya kulelea Watoto yatima, kwa lengo la kuwashika mkono na kuwafariji huwa nafarijika ninapofanya jambo hili ’’,alisema RC Abbas.

Amewapongeza watawa hao kwa upendo mkubwa walionao kwa kuchukua jukumu la kuwahudumia Watoto yatima ambapo amesema jukumu hilo ni la kimungu Zaidi.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Rehema Madenge  amewapongeza watawa hao kwa kwa kuwalea Watoto yatima 74  ambao amesema wanalelewa katika mikono salama kutokana na kituo hicho kuwa kimbilio la Watoto wengi.

Amesema kituo hicho kinaisaidia serikali kulea Watoto yatima na kwamba hakuna malipo yanayostahili kwa kazi hiyo Zaidi ya kuwaombea thawabu kwa mwenyezi Mungu.

Afisa Ustawi Mkoa wa Ruvuma Vikta Nyenza akitoa taarifa ya vituo vya kulelea yatima amesema katika Mkoa mzima kuna Watoto yatima 279 kati yao watoto 74 wanalelewa katika kituo cha Chipole.

Jumuiya ya watawa wa Chipole imemshukuru Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kwa msaada wa vitu na fedha na kuwafariji na kuwatia moyo wa kuendelea kuwa na huruma na upendo wa kuwahudumia Watoto yatima.

## KANALI ABBAS AIPONGEZA MANISPAA YA SONGEA KUTEKELEZA MAAGIZO YA LAAC



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed ameupongeza uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwa kutekeleza maagizo sita kati ya nane yaliyotolewa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) mwaka 2022.

Kanali Abbas ametoa pongezi hizo wakati anazungumza kwenye kikao cha kujadili utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya LAAC kilichofanyika kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea.

Hata hivyo amezitaja hoja za miaka ya nyuma  katika Halmashauri hiyo ambazo bado hazijafanyiwa kazi kikamilifu ili ziweze kufungwa ni 12 na kwamba kuna hoja na mapendekezo 53  ambayo yanatakiwa kufungwa na kufanyiwa kazi.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma pia ameipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kutekeleza maagizo Matano kati ya sita ya Kamati ya LAAC.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea kati ya maagizo matatu yaliyotolewa na LAAC ni maagizo mawili yametekelezwa na kufungwa huku agizo moja utekelezaji wake haujakamilika kwa kipindi cha miaka minne sasa.

“Katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea jumla ya hoja na mapendekezo 44 bado hayajafanyiwa kazi ili yafungwe hivyo nawaomba waheshimiwa madiwani kufanya ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha hoja zote zinajibiwa ipasavyo’’,alisisitiza RC Abbas.

Akizungumza kwa nyakati tofauti katika Halmashauri hizo,Mkuu wa Mkoa ameziagiza Halmashauri hizo kuhakikisha zinafanya maandalizi ya majibu ya hoja mapema na kwamba Halmashauri zichukue mapema hatua za kinidhamu kwa watumishi wanaozalisha hoja.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea Mheshimiwa Menas Komba ameahidi kuhakikisha hoja zote zilizosalia katika Halmashauri hiyo zinajibiwa na kufungwa sanjari na kusimamia kasi ya ukusanyaji wa mapato.

Naye Mstahiki Meya wa Manispaa ya Songea Mheshimiwa Michael Mbano,amesema  Halmashauri imejitahidi kutekeleza maagizo sita ya LAAC  na kwamba maagizo  mawili yaliyosalia itayatekeleza ili yaweze kufungwa.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma amefanya vikao vya kujadili utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya LAAC yaliyotolewa katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 katika Halmashauri za Nyasa,Mbinga Mji, Namtumbo,Halmashauri ya Willaya ya Songea,Manispaa ya Songea na  Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

## WAKURUGENZI WALIVYOKABIDHIANA OFISI SONGEA



Pichani kushoto ni aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea Dkt Federick Sagamiko ambaye amehamia kuwa Mkurugenzi wa Jiji la Tanga akimkabidhi rasmi ofisi Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea Wakili Bashiri Muhoja katika hafla iliyofanyika Manispaa ya Songea

## SERIKALI ILIVYOBORESHA HOSPITALI YA MPITIMBI



Muonekano wa baadhi ya majengo ya hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea iliyojengwa katika kijiji cha Mpitimbi.Hospitali hii imekuwa kimbilio sio tu la wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea bali pia baadhi ya wananchi wa nchi jirani ya Msumbiji wanafika kupata huduma katika hospitali hii



## RC RUVUMA AHIMIZA KASI YA UKUSANYAJI MAPATO



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amewataka watendaji katika Halmashauri zote kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato na kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kukuza uchumi na kuongeza pato la Taifa.

Kanali Abbas ametoa agizo hilo wakati anazungumza kwa nyakati tofauti na madiwani na watendaji wa Halmashauri za Nyasa,Songea,Namtumbo,Mbinga Mji na Halmashauri ya wilaya ya Mbinga katika ziara ya kikazi ya kutembelea Halmashauri hizo ambapo pia amesisitiza kuimarisha uhusiano na nchi jirani za Malawi na Msumbiji

## KATIBU TAWALA RUVUMA AWAFUNDA WATUMISHI WA UMMA



KATIBU Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Rehema Sefu Madenge ametoa rai kwa watumishi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kufanya kazi kwa kuzingatia weledi ili waweze kutoa huduma bora kwa wananchi wanaowahudumia.

Madenge ametoa rai hiyo wakati anazungumza na watumishi hao katika kikao kilichofanyika kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea,lengo kubwa la kikao hicho likiwa ni kujitambulisha rasmi kwa watumishi hao baada ya kuhamia Mkoa wa Ruvuma akitokea Mkoa wa Dar es salaam.

Katibu Tawala huyo amewaasa watumishi hao kufanya kazi kwa Pamoja kama timu,kupendana kwa dhati,kusaidiana na kuelewana ili kutekeleza majukumu kwa ufanisi.

“Kila mmoja afanye kazi kulingana na fani yake, fanyeni kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu,busara na kuzingatia misingi ya utumishi wa umma ikiwemo uwajibikaji'',alisisitiza Madenge.

Madenge amesisitiza kuimarisha usimamizi wa miradi mbalimbali inayotekelezwa katika Mkoa wa Ruvuma na kusimamia sekta ya elimu ambayo haifanyi vema katika Mkoa wa Ruvuma.

Hata hivyo Katibu Tawala huyo ameagiza kuboreshwa kwa mazingira katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kuimarisha usafi katika viunga vya mji wa Songea hali ambayo itavutia watu wengi.

Awali akizungumza kwenye kikao hicho Kaimu Katibu Tawala Msaidizi ,Rasilimali watu Mkoa wa Ruvuma Salum Kateula amesema ofisi ya Mkuu wa Mkoa ina jumla ya watumishi 174 ambao baadhi yao wanafanya kazi katika ofisi za wakuu wa wilaya tano zilizopo mkoani Ruvuma.



*Baadhi ya watumishi wa umma kutoka sektretarieti ya Mkoa wa Ruvuma wakimsikiliza Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Rehema Madenge*

# RC AWAAGIZA MADABA KUTEKELEZA MAAGIZO YA LAAC




MAAGIZO yote sita yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) Oktoba 2022 katika Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma hayajatekelezwa hadi sasa.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Mkuu wa Wilaya ya Mbinga Mheshimiwa Kisale Makoli kwenye kikao cha kujadili utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya LAAC kilichofanyika kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Madaba.

Maagizo hayo ni Pamoja na Halmashauri kuweka mikakati ya kufanikisha ukusanyaji wa mapato ya ndani yasiyopungua sh.bilioni mbili,kulipa kodi ya zuio ya shilingi milioni 24.9 kwa TRA,kusimamia suala la fidia ya sh.milioni 229.8 inayotokana na kuvunjwa kwa mkataba na TBA,kukusanya sh.milioni 8.2 kutoka kwenye vikundi na kufunga mfumo wa GOT-HOMIS kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Kanali Abbas amesema Kamati ya LAAC ilitoa maagizo hayo sita ambayo yalipaswa kutekelezwa kikamilifu na Menejimenti ya Halmashauri hiyo.

“Hali ya utekelezaji hadi sasa hairidhishi kabisa,hakuna agizo hata moja ambalo limetekelezwa na kufungwa,pia mwenendo wa kushughulikia hoja na mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali CAG bado hauridhishi kabisa’’,alisisitiza Kanali Abbas.

Kutokana na hali hiyo Mkuu wa Mkoa amewaomba waheshimiwa madiwani kufuatilia kwa karibu na kuhakikisha hoja zote zinajibiwa ipasavyo na kuweka mikakati ya kuhakikisha hoja hizo hazijirudii tena.

Kanali Abbas amewataka wakuu wa Idara kushiriki ipasavyo katika kuandaa majibu ya hoja na utekelezaji wa mapendekezo ya CAG ambapo ameuagiza uongozi wa Halmashauri hiyo kuchukua hatua mapema za kinidhamu kwa watumishi wanaozalisha hoja.

Katika Halmashauri hiyo hadi sasa kuna jumla ya hoja na mapendekezo 52 ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi ili yafungwe.

Awali Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Rehema Madenge akizungumza kwenye kikao hicho ameuagiza uongozi wa Halmashauri hiyo kuhakikisha wanajitahidi kujibu hoja zote kwa wakati ,kwa usahihi na kushirikiana watendaji wote wa Halmashauri husika kujibu hoja.

Amesisitiza kuwa hoja hizo zinazalishwa na watumishi hivyo watumishi wenyewe wanatakiwa kujibu hoja zote kwa wakati kama ilivyoelekezwa ili Kwenda na muda uliopangwa.

Akizungumza kwa niaba ya waheshimiwa Madiwani,Naibu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Mheshimiwa Oraph Pilly amesema wamesikitishwa na taarifa ya kushindwa kutekeleza kwa wakati maagizo yote sita ya LAAC katika Halmashauri hiyo.

Kutokana na hali hiyo waheshimiwa madiwani hao wamemwomba Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo ifikapo Aprili 5 mwaka huu kufanya kikao maalum cha kuangalia nini kilisababisha kushindwa kutekelezwa maagizo ya LAAC kwa wakati.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Mheshimiwa Teofanes Mlelwa ameridhia kufanyika kwa kikao hicho maalum ambapo amesisitiza kuwa amekosa amani kutokana na Halmashauri hiyo kushindwa kutekeleza maagizo hayo kwa wakati na kwamba amepokea maagizo yote yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa na kuahidi kuyafanyia kazi.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma amefanya vikao vya kujadili utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa yaliyotolewa katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 katika Halmashauri saba za Mkoa wa Ruvuma.

## MUONEKANO WA JENGO LA HALMASHAURI YA MADABA




Muonekano wa jengo la Halmashauri ya Madaba wilayani Songea ambalo limekamilika na kuhudumia watumishi na wananchi,serikali imetoa mabilioni ya fedha kutekeleza mradi huu.

Picha ya chini ni muonekano wa hospitali ya Halmashauri ya Madaba wilayani Songea ,mradi wa hospitali hii umekamilika na kuanza kutoa huduma za afya kwa wananchi hivyo kupunguza kero ya kusafiri Zaidi ya kilometa 200 kwenda na kurudi kufuata huduma za matibabu katika hospitali ya Rufaa ya Songea



## BANDARI YA KIMKAKATI YA NDUMBI KUIFUNGUA NYASA




Serikali imetenga zaidi ya shilingi bilioni 150 kuanza ujenzi wa barabara ya lami nzito kutoka kijiji cha Ruanda Halmashauri ua Wilaya ya Mbinga hadi Bandari ya Ndumbi Halmashauri ya wilaya ya Nyasa hivyo kuendelea kufunguliwa wilaya ya Nyasa katika sekta ya usafiri na usafirishaji.

Serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 12 kujenga bandari ya kimkakati ya Ndumbi katika ziwa Nyasa,mradi huo umekamilkika kwa asilimia 100,pia serikal;i imetenga shilingi bilioni 85 kuanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa bandari ya Mbambabay wilayani Nyasa



## WAKULIMA MBINGA WAZALISHA KAHAWA TANI 20,000



WAKULIMA wa kahawa wanaohudumiwa na Chama kikuu cha Ushirika wilaya ya Mbinga (MBIFACU),katika kipindi cha miaka mitatu wamefanikiwa kuongeza uzalishaji wa zao hilo kutoka tani 12,000 msimu wa kilimo 2020/ 2021 hadi tani 20,000 katika msimu wa kilimo 2023/2024.

Kaimu Meneja wa MBIFACU Faraja Komba amesema, ongezeko la uzalishaji limetokana na mikakati ya Serikali ya awamu ya sita ya kuwainua wakulima.

Amesema,mpango wa serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kutoa pembejeo za ruzuku kwa wakulima umehamasisha na kuwavutia watu wengi kujikita kwenye kilimo cha zao la kahawa.

Komba amesema,katika kipindi cha miaka mitatu wakulima wameongeza takribani tani 8 sawa na kilo milioni 8 ambazo ni mafanikio makubwa katika sekta ya ushirika na wakulima wa kahawa kwa ujumla.

Amesema,kuanzia mwaka 2021 hadi 2024 wametoa mikopo ya mbolea yenye thamani ya Sh.bilioni 11 kwa wakulima wanaojihusisha na kilimo cha kahawa na serikali imeunga mkono kwa kutoa Sh.bilioni 10.6. zilizokwenda kwa wakulima kupitia vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS).

Komba ameishukuru serikali kuboresha masoko ya kahawa,kwani sasa wakulima wanatumia masoko matatu(soko la awali,soko la mnadani na soko la mauzo ya moja ambayo yamesaidia kurahisisha mauzo ya kahawa na wakulima kupata fedha zao kwa wakati.

Amesema,serikali ikiendelea kutoa pembejeo hasa mbolea za ruzuku,uzalishaji wa kahawa katika wilaya ya Mbinga utaongezeka kutoka tani 20,000 na kufikia malengo ya kuzalisha tani 35,000 ifikapo mwaka 2030.

## KISIWA CHA MBAMBABAY CHENYE UTAJIRI WA SAMAKI WA MAPAMBO



Hiki ni kisiwa cha Mbambabay chenye ukubwa wa hekta 27 kilichopo ziwa Nyasa Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma,kisiwa hiki kimebarikiwa kuwa na utajiri mkubwa wa samaki wa mapambo ambapo katika ziwa Nyasa kuna aina zaidi ya 400 wa samaki wa mapambo ambao wamekuwa wanavutia watalii na wageni wanaotembelea wilaya hiyo ambayo ni kitovu cha utalii mkoani Ruvuma.

## PERAMIHO ILIVYOSHEHENI UTALII WA KIHISTORIA



MJI wa Peramiho uliopo Wilaya ya Songea Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa miji ya zamani yenye historia ya kipekee katika ukanda ya kusini.Mji wa huo unafahamika zaidi nje ya nchi pengine kuliko miji mingine iliyopo kusini mwa Tanzania kutokana na mji huo kuwa na historia ya namna yake kipekee ikiunganisha Tanzania na mataifa ya Ulaya.

Historia ya mji wa Peramiho uliopo kilometa 24 tu kutoka makao makuu ya mkoa wa Ruvuma Songea inaunganishwa na wabenediktini wa kanisa katoliki kutoka St.Otilia nchini Ujerumani,ambao waliamua kuweka makao makuu yao katika Abasia ya Peramiho.

Wabeneditine hao waliingia kwa mara ya kwanza katika mji huo mkongwe mwaka 1898 wakiongozwa na Kasian Spiss.Tangu wakati huo wabenediktine hao wamekuwa wakifanya mambo yanayoutangaza mji huo hali iliyosababisha kuutambua mji wa Peramiho kuwa ni mji unaokidhi vigezo kuwa mji wenye utalii wa kiutamaduni.

Kanisa la pili la Peramiho lina saa ya maajabu ambayo ilitengenezwa kwa vyuma zaidi ya miaka 70 iliyopita na wajerumani na kwamba tangu mwaka 1946 ilipotengenezwa hadi sasa saa hiyo haijawahi kusimama wala kupoteza majira jambo ambalo linawashangaza na kuwavutia wengi kutembelea kanisa hilo ili kuiona saa hiyo ya maajabu.

Kanisa kuu la Peramiho lililitumia matofali zaidi ya milioni tatu,ujenzi ulianza wakati Askofu Gallus Steiger na bruda Gisral Stumpf ambaye aliandaa mchoro wa kanisa hilo mwaka 1940 na mwaka 1941 msanii wa majengo Hans Burkard wa Uswis alisanifisha rasimu ya michoro hiyo na kumrejeshea Askofu Gallus mwaka 1943 na michoro kukamilishwa na bruda Gislar.


Kazi ya ujenzi wa kanisa hilo ilianza Julai 6,1943 na kumalizika Septemba 9,1943



## USIYOYAJUA KUHUSU KISIWA CHA LUNDO ZIWA NYASA



Hiki ni kisiwa cha Lundo chenye ukubwa wa hekta 20 kilichopo ziwa Nyasa wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma,kisiwa hiki kimesheheni utajiri mkubwa wa historia ya ya Tanganyika kwa sababu kilitumika na wakoloni wa kijerumani kuhifadhi watu waliopata ulemavu kutokana na ugonjwa wa ukoma baada ya kumalizika vita ya Majimaji ilioanza mwaka 1905 hadi 1907 hivyo wenye ukoma walianza kuhifadhiwa kwenye kisiwa hicho kuanzia mwaka 1908.




**BWAWA LA VIBOKO NAMTUMBO KIVUTIO ADIMU CHA UTALII**



Mkoa wa Ruvuma umebahatika kuwa na vivutio vya aina mbalimbali vya utalii likiwemo bwawa la asili la viboko la Kaunde katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ambalo lina viboko wengi ambao wamekuwa kivutio kikubwa cha utalii.

Wilaya ya Namtumbo imebarikiwa kuwa na vivutio vya utalii ambavyo bado havijatangazwa kikamilifu na kufahamika ili kuvutia watalii na wawekezaji ambao wanaweza kuchangia maendeleo katika sekta ya utalii mkoani Ruvuma.

## DARAJA LA MITOMONI MTO RUVUMA KUANZA JUNI 2024



Serikali ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya kuanza ujenzi wa daraja la Mitomoni katika Mto Ruvuma linalounganisha Wilaya ya Songea na Nyasa mkoani Ruvuma.

Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Innocent Bashungwa akizungumza bungeni Dodoma amesema Wizara hiyo ipo mbioni kuanza kujenga daraja la kisasa na la kudumu katika eneo hilo linalounganisha vijiji vya Mitomoni wilayani Songea na Kijiji cha Mipotopoto wilayani Nyasa.

“Maandalizi ya nyaraka kwa ajili ya kutangaza zabuni kwa mara ya pili kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Mitomoni yamefikia hatua za mwisho na zabuni zitatangazwa mwezi Juni mwaka huu’’,alisema Bashungwa.

Waziri Bashungwa amesisitiza kuwa serikali ya Rais Samia ipo na wananchi wa Wilaya ya Nyasa na Songea na kwamba kufikia Juni mwaka huu ujenzi wa daraja hilo unatarajia kuanza.

# BILIONI 34 ZILIVYOBORESHA SEKTA YA ELIMU RUVUMA



Serikali ya Awamu ya sita imetoa zaidi ya shilingi bilioni 34 kuboresha sekta ya elimu mkoani Ruvuma

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesema fedha hizo zimetumika kuboresha mazingira ya kufundishia na ya kujifunzia kwa kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu kwa lengo la kuhakikisha watoto wanapata elimu katika mazingira bora na yenye staha,

Amesema Fedha hizo zimetumika katika ujenzi wa mabweni 35, matundu ya vyoo 1444, vyumba vya madarasa 301,nyumba za walimu tisa na vichomea taka 12.

Ameongeza kuwa fedha hizo pia zimetumika kujenga shule mpya 21 za sekondari ,majengo ya utawala 12 na vituo vya walimu 12.

Hata hivyo amesema Mkoa wa Ruvuma kwa kipindi cha miaka mitatu umepokea walimu wa ajira mpya 877 ambapo kati yao walimu wa shule za msingi walikuwa 489 na sekondari 388

## SERIKALI YATOA MILIONI 826 KUKAMILISHA MIUNDOMBINU YA ELIMU TUNDURU



Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma imepokea jumla ya shilingi milioni 826 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo katika shule za sekondari wilayani humo.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo Chiza Marando amezitaja shule Shule zilizonufaika na fedha hizi ni pamoja na Shule ya Sekondari Nandembo, Shule ya Sekondari Tunduru, Shule ya Sekondari Masonya, Shule ya Sekondari Mataka, Shule ya Sekondari Matemanga, Shule ya Sekondari Tarajali Kata ya Mbatin a Shule ya Sekondari Tarajali Kata ya Ngapa

" Tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kuhakikisha inaboresha miundombinu ya elimu wilayani Tunduru, fedha hizi zitasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza upungufu wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo katika shule za sekondari'',alisema Marando.

Ametoa rai kwa wataalamu,wasimamizi wa miradi na wakandarasi waliopata zabuni ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo kuhakikisha wanatekeleza miradi hiyo kwa ubora na kwa wakati.

## HOSPITALI YA TUNDURU ILIVYOBORESHA HUDUMA ZA AFYA



Wananchi wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma wameishukuru Serikali ya awamu ya sita kwa kuboresha mazingira ya utoaji wa huduma za afya katika hospitali ya Wilaya, huduma ambazo hapo awali walilazimika kuzifuata nje ya Wilaya ya Tunduru.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru Chiza Marando amesema Hospitali ya Wilaya ya Tunduru imepata mabadiliko makubwa baada ya kukarabatiwa na kwamba Ukarabati huo umesaidia kuboresha huduma za afya na kuleta ahueni kubwa kwa wananchi wa wilaya ya Tunduru.

Amesema wananchi wa Tunduru hivi sasa wanaweza kupata huduma bora za afya karibu na makazi yao.

Marando amesema serikali imetoa kiasi cha shilingi milioni 900 ambazo zimetumika kuboresha miundombinu ya hospitali, vifaa vya tiba, na mazingira kwa ujumla.

Amesema fedha hizo pia zimetumika kujengo jengo la wagonjwa wa nje (OPD),Maabara pamoja na ukarabati wa jengo la upasuaji .

Mkurugenzi Mtendaji huyo amesema Hospitali ina vifaa vya kisasa vya tiba, na vifaa vya kufuatilia afya ya wagonjwa.

Mganga Mkuu wa Wilaya wa Hospitali ya Tunduru, Dk.Wilfred Rwechungura amesema kukamilika kwa mradi huo kumepunguza changamoto kubwa ya

uchakavu wa miundombinu katika Hospitali  na kurahisisha utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi wa wilaya ya Tunduru.

## ELIMU ILIVYOPUNGUZA MADHARA YA TEMBO NAMTUMBO



Diwani wa kata ya Likuyu Wilayani Namtumbo Mkoani Ruvuma Mheshimiwa Kassimu Gunda amewashauri viongozi wa Serikali Kuwajenga wananchi kisaikolojia kwenye migogoro kati ya binadamu na wanyamapori.

Akizungumza kwenye mkutano wa hadhara na wananchi wa Kata ya Likuyu,Gunda amesema ipo tabia ya viongozi kutojitokeza kwenye migogoro kati ya wanyamapori na binadamu hasa inapotokea binadamu kuuawa na tembo kwa kuogopa Wananchi kuwa na hasira Kwa viongozi wao.

Gunda ameitaja faida ya viongozi kuwa na wananchi wakati wa matatizo yao kunawajenga wananchi kisaikolojia  hivyo kushirikiana nao bega Kwa bega kwenye changamoto mbalimbali .

Diwani huyo ameiomba serikali Kuharakisha kifutajasho kwa wananchi pale wanapoathirika na tembo ili wananchi walioathirika na wanyamapori waweze Kununua chakula ambacho kiliharibiwa na wanyamapori hao.

Hata hivyo Menas Fusi Mkazi wa kitongoji cha Mfuate Kijiji Cha Likuyu amesema kasi ya tembo kwenda katika mashamba ya wakulima imepungua Kutokana na kuwepo Kwa Jeshi la TANAPA ambalo Kwa kiasi kikubwa hufanya kazi ya kuwarudisha tembo hao katika hifadhi .

Afisa Maliasili na Utalii wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo Priska Msuha amesema Licha ya kutokea Changamoto ya tembo mmoja mwenye mtoto kumua mwananchi katika Kijiji Cha Likuyu hivi karibuni, changamoto ya tembo imepungua Kutokana na Kambi ya TANAPA kufanya kazi kubwa ya kuwarudisha wanyamapori hao hifadhini.

Afisa Maliasili huyo amesema ofisi yake inaendelea kutoa elimu ya namna ya kukabiliana na wanyamapori kama tembo ambapo hivi sasa wananchi wakimwona tembo hawamfuati hubaki kimya badala yake wanapiga simu kwa Mamlaka zinazohusika ambao hufika kuwaondoa tembo hao katika makazi ya watu

## DC NYASA AWAASA WANANCHI KUJITOKEZA UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA



Mkuu wa Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma Mheshimiwa Peres Magiri, amewataka wananchi wa Wilaya ya Nyasa kushiriki kikamilifu Uchaguzi wa Serikali za mitaa unaotarajia kufanyika mwaka huu 2024.

Ameyasema hayo wakati anazungumza na wananchi katika Kijiji cha Ndengere Kata ya Mbambabay ambapo pia alitumia nafasi hiyo kujitambulisha kwa wananchi, kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua.

Magiri amewaeleza wananchi hao kuwa mwaka huu kutakuwa na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa hivyo wananchi, wanatakiwa kushiriki kwa kujitokeza kugombea na kuchagua viongozi bora watakaowaletea maendeleo.

“Ushiriki wa wananchi ni muhimu sana Katika Uchaguzi wa mwaka huu ili kuchagua viongozi bora, ngazi ya chini ambao watapunguza malalamiko na kero za wananchi katika Ngazi ya Vijiji na Kata’’,alisisitiza.

Ametoa rai kwa makundi maalum kama wanawake,wenye ulemavu na vijana kushiriki kikamilifu kwenye uchaguzi wa mwaka huu,ikiwa ni Pamoja na kuchukua fomu za kugombea nafasi za Uongozi.

## OFISI YA RC RUVUMA YAPOKEA MIPIRA 1,000 TOKA TFF




OFISI ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma imepokea mipira 1000 iliyotolewa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kupitia program ya Football For Schools kwa ajili ya kuendeleza michezo katika shule za msingi na sekondari.

TFF imetoa mipira hiyo ikiwa ni jitihada za Rais wa Shirikisho hilo kumuunga mkono Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan katika kuendeleza michezo nchini Tanzania.

Akizungumza kwenye hafla hiyo kabla ya kukabidhi vifaa hivyo,Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amewashukuru TFF na kumpongeza Rais Samia kwa kuwa mstari wa mbele katika kuendeleza na kukuza sekta ya michezo.

“Rais Samia ana maono makubwa ya kuhakikisha Tanzania inafanya vizuri katika michezo ya ndani na nje ya mipaka ya nchi’’,alisisitiza.

Hata hivyo amesema Mkoa wa Ruvuma umekuwa na maendeleo ya wastani katika michezo ambapo ameupongeza uongozi wa Chama Cha Mpira wa Miguu mkoani Ruvuma FARU kwa kuwa mstari wa mbele kupigania maendeleo ya soka kwa wanawake.

Katika hafla hiyo jumla ya mipira 800 kati ya 1000 iligawiwa katika shule za msingi na sekondari zilizopo katika Halmashauri nane za Mkoa wa Ruvuma,

## WADAU WALIVYODHAMIRIA KUSIMAMIA MFUMO WA STAKABADHI NAMTUMBO



Kikao Cha wadau katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo Mkoani Ruvuma kimeazimia kusimamia mfumo wa stakabadhi ghalani Wilayani humo kutokana na mfumo huo kuonesha mafanikio makubwa kwa wakulima.

Kikao hicho kimehudhuriwa na Viongozi wa vyama vya msingi 47 katika Wilaya ya Namtumbo , viongozi wa vikundi vya wakulima ,wanunuzi wa mazao ,viongozi wa wafanyabiashara ,kamati ya Ulinzi na usalama ya Wilaya ya Namtumbo ,wakuu wa idara , Taasisi za kibenki Pamoja na wamiliki wa maghala.

Akitoa taarifa ya uendeshaji mfumo wa stakabadhi ghalani Kwa msimu uliopita wa mwaka 2022/2023 Afisa Kilimo,Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo Paul Ambokile amesema mauzo kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani umewanufaisha wakulima Kwa kiasi kikubwa.

Mwenyekiti wa Chama Cha Msingi Namtumbo Asedi Kaporo amesema kuwa mfumo wa stakabadhi ni mzuri kwa kuwa wakulima wanauza mazao yao kwa bei kubwa tofauti na soko holela ambalo limekuwa linawanyonya wakulima.

Diwani wa Kata ya Mkongo Mheshimiwa Daniel Nyambo amesema mfumo wa stakabadhi ghalani unawanufaisha wakulima ambapo ametoa rai kwa wadau hao kuwadhibiti wafanyabiashara ambao hukopesha wakulima fedha ndogo na hulipwa ufuta mwingi na wao kuuza katika mfumo wa stakabadhi ya ghala na kujipatia pesa nyingi.

Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo Mheshimiwa Ngollo Malenya amesema mfumo wa stakabadhi ghalani umewawezesha wakulima wa Wilaya ya Namtumbo kupata bei nzuri Kwa mazao ya ufuta,mbaazi na soya Pamoja na kuwa na uhakika wa soko.

Amewaagiza viongozi wa vyama vya msingi kuhakikisha wanasimamia mfumo Kwa uadilifu mkubwa na kusisitiza kuwa serikali itaendelea kusimamia haki na maslahi ya wakulima .

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo Philemon Magesa amewataka wadau kushirikiana katika kuhakikisha mfumo wa stakabadhi ghalani una wanufaisha wananchi wa Namtumbo.

## MILIONI 69 KUJENGA KITUO CHA ASKARI WANYAMAPORI NAMTUMBO



HALMASHAURI ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma imetenga shilingi milioni 69 kujenga kituo cha askari wanyamapori katika kijiji cha Nambecha ili kukabiliana na Wanyamapori.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo Mheshimiwa Ngollo Malenya wakati anazungumza na wananchi wa kijiji cha Nambecha kufuatia malalamiko ya wakulima waliovamiwa na tembo kwenye mashamba yao.

Amesema kukamilika kwa jengo hilo kutaimarisha Usalama wa wananchi na mazao katika vijiji vyote ambavyo vipo karibu na hifadhi za Wanyamapori.

# SERIKALI YAFIKISHA UMEME VIJIJI 81 NYASA



SERIKALI imetatua kero ya umeme katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma baada ya kufikisha huduma ya umeme katika vijiji 81 kati ya vijiji 84 vilivyopo wilayani humo.

Mkuu wa Wilaya ya Nyasa Mheshimiwa Peres Magiri amesema katika Wilaya ya Nyasa vimebakia vijiji vitatu ambavyo bado havina umeme ambavyo Mkandarasi yuko kazini anaendelea na kazi ya kupelaka Umeme katika vijiji hivyo.

Magiri ameyasema hayo wakati anazungumza na Wananchi wa Kijiji cha Ndengere Kata ya Mbamba bay Wilayani Nyasa.

Amewataka wananchi ambao hawajapata huduma ya umeme kuwa wavumilivu kwa kuwa nia ya Serikali ni kufikisha umeme katika ngazi ya kila kijiji na awamu itakayofuata ni kufikisha umeme katika ngazi ya Kitongoji.

“Serikali yetu ni Sikivi kama imeweza kupeleka umeme katika Vijiji 81 katika Wilaya ya Nyasa haitashindwa kufikisha umeme katika Vitongoji’’,alisisitiza.

# NFRA YAWAFUNDA WAKULIMA SONGEA




WAKULIMA wa mahindi mkoani Ruvuma,wamekumbushwa umuhimu wa kufuatilia maendeleo ya mazao yao mashambani na kuhakikisha wanavuna mazao yaliyokomaa ili kupata soko la uhakika.

Wito huo umetolewa na Meneja wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya chakula (NFRA) Kanda ya Songea Zenobius Kahere, wakati akizungumzia maandalizi ya ununuzi wa mahindi katika msimu wa kilimo 2024/2025 ofisini kwake mjini Songea.

Amesema,hatua hiyo itawezesha NFRA kupata nafaka bora kwa ajili ya akiba ya chakula kwa wananchi watakaopatwa na upungufu wa chakula katika maeneo yao.

Kwa mujibu wa Meneja huyo,katika msimu wa mwaka huu NFRA itanunua mahindi kwa kuwahusisha wakulima wakubwa,wafanya biashara wakubwa na wakulima wadogo.

Amebainisha kuwa,wakulima wakubwa waliokusudiwa katika mpango huo ni wakulima wanaoanza na hekari 100 na wenye uwezo wa kuuza tani 200 na kuendelea.

“Kwa upande wa wafanya biashara ni wale wenye uwezo wa kununua mahindi kutoka kwa wakulima kuanzia tani 2,000 hadi 5,000”.

Amevitaja,vigezo vilivyowekwa kwa wakulima wakubwa watakaotaka kuuza mahindi kwa Serikali kuwa ni lazima atoke kwenye Halmashauri anayofanyia shughuli zake za kilimo ili NFRA iweze kumpa mkataba wa kuuza mazao yake kama mkulima na siyo vinginevyo.

Hata hivyo amesema,wafanyabiashara wakubwa watalazimika kuwa na barua ya utambulisho kutoka kwa Halmashauri ya wilaya wanakofanyia biashara zao ili muda utakapofika wa kuanza kununu nafaka iwe rahisi kwa NFRA kuweka usimamizi mzuri wa upatikanaji wa nafaka hiyo.

## DKT NCHIMBI AKABIDHI VIFAA VYA USAFIRI KWA VIONGOZI WA CCM MADABA



Katibu Mkuu wa CCM Taifa Dkt. Emanuel Nchimbi akikabidhi vyombo vya usafiri vilivyotolewa na Mbunge wa Jimbo la Madaba Dkt Joseph Mhagama miongoni mwa viongozi wa matawi katika hafla iliyofanyika mjini Madaba

Katibu Mkuu wa CCM yupo mkoani Ruvuma kwa ziara ya kikazi ya siku tano.

## KATIBU MKUU AAGIZA UWEKEZAJI KWENYE MICHEZO



Katibu Mkuu wa CCM Taifa Balozi Dkt Emanuel Nchimbi ameagiza sekta ya michezo kuendelezwa kwa kuwa watanzania wengi wakiwemo wakazi wa Mkoa wa Ruvuma wanapenda michezo.

Dkt. Nchimbi ameyasema hayo alipokuwa akizungumza na wananchi wa Mkoa wa Ruvuma katika ziara yake mjini Songea.

Dkt Nchimbi amesikitishwa namna ambavyo viongozi wa Michezo Mkoa wa Ruvuma walivyo kwamisha Maendeleo ya michezo.

Hata hivyo Balozi Dkt. Nchimbi amebainisha baadhi ya mifano ambayo yeye alipokuwa Mbunge wa jimbo la Songea mjini alishuhudia ikiwemo viongozi wa Timu ya Mkoa wa Ruvuma ya Majimaji FC kuhujumiwa na baadhi ya viongozi wa wakati huo wa Timu ya Majimaji Fc

Katibu Mkuu huyo amewataka Watanzania kwa ujumla kuacha tabia za ubadhirifu na wizi hasa katika michezo ili kuendelea kuboresha michezo nchini.

## MADAKTARI BINGWA KUTOA HUDUMA ZA KIBINGWA SONGEA



Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea, Dr. Magafu Majura amesema kuwa wanatarajia kupokea jopo la madaktari bingwa kutoka Hospitali za Rufaa za mikoa ya nyanda za juu kusini ambayo Ruvuma, Njombe, Mbeya na Songwe.

Akizungumza ofisini kwake amesema kuwa wanatarajia kupokea madaktari bingwa ambao watatoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea (HOMSO).

Dr.Majura amesema katika kambi hiyo kutatolewa huduma mbalimbali za kibingwa za akina mama na uzazi, huduma za magonjwa ya watoto, huduma za kibingwa za magonjwa ya ndani kama vile kisukari, shinikizo la damu, figo na moyo, huduma za upasuaji na mifupa, huduma za macho, huduma za Afya ya akili, huduma za kinywa na meno, huduma za masikio, pua na koo, huduma za ngozi, huduma za mfumo wa chakula, huduma za moyo kwa watoto, huduma za saratani.

“Kutokana na uhaba wa huduma hizo Wananchi wamekuwa wakisumbuka kufuata matibabu ya kibingwa mbali hivyo Serikali ya Dkt Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Ruvuma imesogeza huduma karibu ili kuondoa usumbufu kwa Wananchi” amesema Dr. Majura

Amesema ujio wa madaktari hao utakuwa ni fursa kwa wataalamu wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea (HOMSO) kwa sababu watawajengea uwezo wataalamu waliopo.

Dr. Majura amewahimiza wananchi kufika na kupata huduma na kwamba kutakuwepo na wataalamu wa huduma za mionzi za damu za usingizi na ganzi.

## MBINGA WAVUNJA REKODI MAPOKEZI YA KATIBU MKUU CCM



KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi Taifa Balozi Dkt.Emanuel Nchimbi ameendelea na ziara yake mkoani Ruvuma kwa kutembelea wilaya ya Mbinga ambako wanachama wa CCM na wananchi wa Mbinga wamejitokeza kwa wingi kwenye eneo la mapokezi hoteli maarufu mkoani Ruvuma ya One Pacific.Katibu Mkuu katika ziara hiyo ameongozana na Katibu wa Taifa wa Itikadi,Uenezi na mafunzo Ndugu Amosi Makalla wakiwa na Mwenyeji wao Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed

## KATIBU MKUU CCM ALIVYOPOKEWA KIMILA SONGEA



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt Emmanuel Nchimbi amekaribishwa rasmi nyumbani kwao Mkoa wa Ruvuma kwa kufanyiwa kimila na machifu pamoja na wazee wa jadi alipofika eneo la Mnara wa Kumbukumbu ya Mashujaa wa Vita ya Maji Maji mjini Songea.

Katika ziara hiyo, Dkt. Nchimbi ameambatana na wajumbe wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM (NEC), Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla pamoja na Katibu wa Oganaizesheni, Issa Haji Gavu.

Kiongozi huyo Mtendaji MKuu wa CCM, amekuwa na ziara ya kikazi ya siku tano mkoani Ruvuma ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya siku 10 katika mikoa ya Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Ruvuma.

Lengo la ziara hiyo ya mikoa sita iliyohitimishwa mkoani Ruvuma lilikuwa ni kuimarisha uhai wa chama, kutatua kero za wananchi, kuelezea maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani, kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya chama hicho.

## DKT NCHIMBI AZURU KABURI LA MUASISI WA TANU MBINGA



Katibu Mkuu wa CCM, Dkt. Emmanuel Nchimbi amezuru kaburi la mmoja wa waasisi wa chama cha TANU (Ambacho kiliungana na chama cha ASP mwaka 1977 na kuanzishwa CCM) Costantine Osward Millinga (LIKAPU) aliyefariki Machi 5, 2018 wilayani Mbinga mkoani Ruvuma.

Mbali ya kuzuru kaburi hilo na kuweka shada la maua, Dkt. Nchimbi alifika nyumbani kwa marehemu na kutoa pole kwa mjane Maria Costantine Millinga na kusaini kitabu cha kumbukumbu akiwa hapo.

Akiwa hapo, Dkt. Nchimbi ameahidi CCM kuendelea kuenzi mema yaliyofanywa na waasisi wa TANU pamoja na kuwaenzi wote waliosaidia kwenye kuanzishwa kwake na kubeba dhamana ya kupigania uhuru wa Tanganyika ambao ulichangia kupatikana kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1964.

Enzi za uhai wake, marehemu Likapu aliyefariki akiwa na umri wa miaka 93 alikuwa mmoja wa washauri wa chama hicho.

# KATIBU MKUU AZURU KABURI LA KEPTENI KOMBA LITUHI



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk Emmanuel John Nchimbi, amezuru kaburi la Hayati Kepteni (mst) John Damiano Komba na kutoa heshima zake kwenye kaburi hilo kwa kuweka shada la maua.

Dkt. Nchimbi ambaye ameambatana na Katibu wa NEC – Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM Taifa Amos Makalla pamoja na Katibu wa NEC – Oganaizesheni wa CCM Taifa Issa Haji Gavu, pia alipata wasaa wa kuwasalimia na kuwapatia pole familia, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wa Kijiji cha Lituhi, alipozikwa Kepteni Komba.

Hayati Komba, ambaye alikuwa mhamasishaji mkuu wa CCM, akiwa pia amefanya kazi kubwa ya nchi, kupitia kazi za sanaa, na aliwahi kuwa Mbunge wa Majimbo ya Mbinga Magharibi na Nyasa, kwa nyakati tofauti, kwa tiketi ya CCM, alifariki dunia mwaka 2015 tarehe 28 mwezi Februari.

Akiwa hapo Lituhi, Dkt. Nchimbi, amekutana na familia na wananchi wa maeneo ya karibu waliojitokeza kuungana nae katika kuzuru kaburi la Komba na kumuombea apumzike kwa amani.

## WANAWAKE 6,500 HUFARIKI KILA MWAKA KWA SARATANI



WANAWAKE Zaidi ya 9,500 kati ya 100,000 hugundulika kila mwaka kuwa na tatizo la saratani ya mlango wa kizazi,kati yao wanawake 6,500 hufariki dunia kila mwaka.

Hayo yamesemwa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Dr.Louis Chomboko wakati anatoa taarifa ya maadhimisho ya wiki ya chanjo na uzinduzi wa dozi moja ya chanjo dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi (HPV) kwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea.

Dr.Chomboko amesema inakadiriwa wanawake Zaidi ya 450,000 wamethibitika kuwa na saratani ya mlango wa kizazi duniani na wengi wao wapo katika nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania.

“Saratani ya mlango wa kizazi inashika nafasi ya pili kwa kusababisha saratani kwa wanawake ulimwenguni,nafasi ya kwanza inashikwa na saratani ya matiti’’,alisisitiza.

Hata hivyo Dr.Chomboko amesema hapa nchini saratani ya mlango wa kizazi inaongoza miongoni mwa saratani zote zinazogundulika miongoni mwa wanawake wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 44.

Ameyataja mambo yanayochochea kupata saratani ya mlango wa kizazi kuwa ni kuanza kujamiana katika umri mdogo,kuwa na wapenzi wengi,kuwa na ndoa za

mitaala,uvutaji sigara,kuwa na mpenzi asiyetahiriwa na virusi vya UKIMWI na UKIMWI.

Amezitaja dalili za saratani ya mlango wa kizazi kuwa ni kutokwa damu bila mpangilio,maumivu ya mgongo,kuchoka,kutoka uchafu kwenye uke, kuishiwa damu,figo kushindwa kufanya kazi, uvumbe wa tezi na kupatwa na fistula.

Ii kujikinga dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi,Mganga Mkuu huyo wa Mkoa wa Ruvuma amesema ni vema kupata chanjo ya kuzuia saratani hiyo,kubadili tabia,kuepuka ngono katika umri mdogo,kuepuka uvutaji sigara na kuwa na mwenzi mmoja mwaminifu.

Akizungumzia huduma za kupima na kutibu saratani ya mlango wa kizazi katika Mkoa wa Ruvuma,Dr.Chomboko amesema Mkoa una jumla ya vituo 59 vinavyotoa huduma ya upimaji wa saratani ya mlango wa kizazi na kwamba kati ya hivyo vituo 30 vina mashine za matibabu ya saratani ya mlango wa kizazi.

Amesema katika mwaka 2023,jumla ya wanawake 13,825 walichunguzwa na kati yao wanawake 348 waligundulika kuwa na viashiria vya awali vya saratani ya mlango wa kizazi na kwamba wanawake 313 walipatiwa tiba na wanawake 119 walihisiwa kuwa na saratani ya mlango wa kizazi.

Hata hivyo amesema wanawake 70 walithibitika kuwa na saratani ya mlango wa kizazi ambao walipata rufaa.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed akizungumza kabla ya kuzindua maadhimisho hayo amesema Mkoa wa Ruvuma unatarajia kutoa chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi kwa wasichana wenye umri wa kuanzia miaka tisa hadi 14 wapatao 147,447.

Ameitaja kaulimbiu ya wiki ya chanjo mwaka 2024 kuwa ni Jamii iliyopata chanjo yenye afya ambapo ametoa rai kwa jamii nzima kuhakikisha walengwa wote wanapata fursa ya kupata chanjo hiyo.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Rehema Madenge ametoa rai kwa viongozi wa dini na watendaji katika ngazi zote kuendelea kuwahamasisha wazazi na walezi wenye Watoto walengwa ambao bado hawajapata chanjo hiyo kuhakikisha Watoto wao wanapata chanjo hiyo muhimu.

Chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi mkoani Ruvuma imeanza kutolewa kuanzia Aprili 22 na inatarajia kukamilika Aprili 28 mwaka huu.

## WEZI NDANI YA MAGARI WANASWA SONGEA



Jeshi la Polisi mkoani Ruvuma limefanikiwa kumkamata Alpher Christophrer Minja mkazi wa eneo la Sanawali jijini Arusha ambaye alikuwa akitafutwa kwa muda mrefu kwa makosa ya unyang'anyi na wizi ndani ya magari ambayo yalikuwa yanaegeshwa maeneo mbalimbali ya hoteli,nyumba za kulala wageni na kwenye kumbi za starehe Manispaa ya Songea.

Akizungumza na waandishi wa habari Kamanda wa Polisi Mkoani Ruvuma Marco Chilya amesema kuwa kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko kuwa watu wakiwa kwenye maeneo hayo wakiwa wameegesha magari yao na kutoka kwenda kwenye hoteli au kumbi za starehe walikuwa kuibiwa mali zao walizokuwa wamezihifadhi kwenye magari yao jambo ambalo lilikuwa kero kubwa kwa wakazi wa Songea.

Amebainisha kuwa Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama walifanikiwa kupata upelelezi wa kina ambao ulisababisha kupatikana kwa mtuhumiwa ambaye alikuwa akitafutwa kwa muda mrefu na kwamba baada ya mahojiano ya awali na Polisi imebainika kuwa mtuhumiwa Minja alitokea mkoani Arusha na alifika Songea mkoani Ruvuma na kufanya matukio ya unyang'anyi na wizi wa mali za raia ambazo walikuwa wamezihifadhi kwenye magari yao.

Amesema mtuhumiwa Minja baada ya kumuhoji kwa kina zaidi kuhusiana na matukio hayo imebainika kuwa alikuwa na wenzake watatu ambao majina yao yamehifadhiwa kwa upelelezi zaidi wanaodaiwa kuwa walikuwa wakisaidiana na Minja kufanya uhalifu kwenye maeneo ya kumbi za starehe, Hoteli, nyumba za kulala wageni na baa mjini Songea.

Kwa mujibu wa Chilya Minja amekamatwa kwa makosa ya unyang' anyi na wizi ndani ya magari yaliyo kuwa yameegeshwa kwenye maeneo mbalimbali akiwa na jumla ya Laptop 10 mali ambazo zilikuwa zimeibiwa maeneo tofauti mjini Songea na kwamba mtuhumiwa Minja anatarajiwa kufikishwa mahakamani yeye pamoja na watuhumiwa wenzake watatu mara tu baada ya upelelezi kukamilika.

**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA**

**Kupitia Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma**

**S.L.P 74 SONGEA**

**57180 RUVUMA**
**SIMU Nambari.025- 2602256/2602238**
**FAX Na.2602144**
**E-MAIL:** ras.ruvuma@tamisemi.go.tz
**TOVUTI:www.ruvuma.go.tz**
**INSTAGRAM; rs ruvuma**
**FACEBOOK: rs ruvuma**
**YOUTUBE:rs ruvuma**